

Usimamizi wa Vifaa (FM) Taarifa za Tahadhari ya UVA kwa Wachuuzi/Watoa Huduma wasio na Akaunti za UVA

1. Iwapo unafanya kazi na wachuuzi wa ndani au watoa husuma, tafadhali wape tarrifa ifuatayo.

- Kagua taarifa hiyo kwenye [Tahadhari za UVA kwa Usimamizi | wa Dharura wa Umma](#) kwenye tovuti ya (virginia.edu) na fuata_ Maelekezo ya "kuingia" ili kupokea taarifa za Tahadhari ya UVA kupitia ujumbe mfupi wa maandishi.
 - Wote ambao wanajiunga watapokea taarifa kwa siku 365.
 - Huduma ya kujiunga inapokwisha muda wake, waliojiunga waapokea ujumbe mfupi wa maandishi ukiwaalika kujiunga tena.
- Sehemu ya "Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara" pia inaweza kupatikana kwenye tovuti hiyo.

2. Hakikisha wachuuzi na watoa huduma wanatambua Tahadhari za Sauti za King'ora na kuelewa maana zake. [Muhtasari wa mifumo ya king'ora](#) unapatikana kwenye tovuti ya Usimamizi wa Dharura.

3. Wachuuzi na watoa huduma wanapaswa kufuata mwongozo uliotolewa katika tahadhari. Waepuke maeneo yaliyoonyeshwa isipokuwa nafasi ya kazi yao inawahitaji kukabiliana.

- Iwapo hakuna uhakika, wanapaswa kuwasiliana na wasimamizi wao kabla ya kuingia eneo lililotambuliwa.
- Kumbuka: Taarifa za tahadhari zinapaswa kutumwa kila baada ya dakika 15 hadi ujumbe wa mwisho wa "HALI SHWARI" utakapotumwa.

4. Iwapo wapo katika eneo lililotambuliwa katika tahadhari:

- Wanapaswa kufuata mwongozo wa tahadhari.
- Iwapo hawawezi kutoka katika eneo hilo na/au wamejeruhiwa, wanapaswa kupiga simu 911.
 - Taja majina yao, mahali na elezea hali hiyo.
 - Wanapaswa kufuata maelekezo ya mwongozaji wa 911.

5. Hakikisha wachuuzi na watoa huduma wanajua wanachopaswa kufanya iwapo Tahadhari ya UVA imemtambua mshambuliaji amilifu.

- Tazama Video ya [Mafunzo ya UVA ya Uzuiaji na Ukabilianaji wa Mshambuliaji Amilifu](#) __kwenye_tovuti ya UVA ya Idara ya Usalama na Ulinzi._

6. Iwapo Tahadhari ya UVA imetambua kuwa tishio la mshambuliaji amilifu linatokea, ujumbe unaweza kuonyesha "KUKIMBIA, KUJIFICHA, KUPAMBANA". Huo hapo chini ni ufafanuzi wa kila kitendo na hatua zinazopaswa kuchukuliwa.

- Kimbia – Iwapo mshambuliaji amilifu yupo katika eneo lako:
 - Ondoa iwapo kuna njia salama.
 - Acha vitu vyako.
 - Iwapo ni salama kwako kufanya hivyo, wasaidie wengine kukimbia.
 - Iwapo ni salama kwako kufanya hivyo, piga simu 911 kuripoti tukio hilo na eneo lako.
 - Iwapo ulimwona mshambuliaji, toa taarifa ya kutosha kadiri uwezavyo kwa 911, ikiwemo maelezo ya umbo, rangi ya nguo zao na uelekeo wao wa safari.
- Jifiche – Iwapo si salama kutoroka, jifiche katika sehemu isiyoonekana.
 - Lengo lako ni kuifanya sehemu hiyo ionekane haina mtu.
 - Funga mlango kwa kufuri na/au zuia.
 - Funga vioo vya dirisha iwapo inawezekana.
 - Zima sauti ya simu yako na wahimize wengine kufanya hivyo.
 - Zima mianga na simu.
 - Kaa nyuma ya vitu vigumu, mbali na mlango
 - Endelea kukaa kimya na wahimize wengine kufanya hivyo.
 - Eneo lako la kujificha linapaswa kuwa:
 - Lisiloweza kuonekana na mshambuliaji.
 - Linalotoa ulinzi.
- Pigana – Kama suluhisho la mwisho na iwapo tu maisha yako yako kwenye hatari:
 - Jaribu kumdhhibiti mshambuliaji.
 - Iwapo inawezekana, pigana kama kundi.

8. Ni muhimu kukumbuka kuwa lengo la kwanza wasimamizi wa sheria kumpata mshambuliaji na kutuliza hali lakini jua kwamba msaada uko njiani.

- Msimamizi wa sheria anapowasili:
 - Endelea kuwa mtulivu na fuata maelekezo.
 - Mikono yako ionekane wakati wote.
 - Epuka kuashiria au kupiga kelele.

- 8. Unapojikinga katika eneo la Viwanja, na unajihisi salama:
 - Wasiliana na 911 ili kuripoti majeruhi wowote katika eneo lako.
 - Elezea hali hiyo.
 - Tambua mahali ulipo.
 - Fuata maelekezo ya mwongozaji.
 - Kumbuka kuzima kengele ya simu yako ili kuepuka kuvutia watu eneo lako.